

**Swahili A: literature – Standard level – Paper 2**  
**Swahili A : littérature – Niveau moyen – Épreuve 2**  
**Swahili A: literatura – Nivel medio – Prueba 2**

Tuesday 1 May 2018 (morning)

Mardi 1 mai 2018 (matin)

Martes 1 de mayo de 2018 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

**Instructions to candidates**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the part 3 works you have studied and compare and contrast these works in response to the question. Answers which are not based on a discussion of at least two part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is **[25 marks]**.

**Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. En basant votre réponse sur au moins deux des œuvres de la troisième partie que vous avez étudiées, vous devez comparer et opposer ces œuvres dans le cadre du sujet. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la troisième partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à apporter des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[25 points]**.

**Instrucciones para los alumnos**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Conteste una sola pregunta de redacción. Base su respuesta en al menos dos de las obras estudiadas de la parte 3, comparándolas y contrastándolas en relación con la pregunta. Las respuestas que no se basen en al menos dos obras de la parte 3 no recibirán una puntuación alta.
- No está permitido traer copias de las obras estudiadas a la sala de examen.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[25 puntos]**.

Jibu swali **moja** tu la insha. Jibu lako lazima liegemee kwenye **angalau** kazi **mbili** za Sehemu ya 3 ulizojifunza na **ulinganishe na ulinganue** kazi hizi katika kujibu swali. Majibu ambayo hayajadili angalau kazi mbili za Sehemu ya 3 **hayatatuzwa** alama za juu.

### Tamthilia

1. Kuwasilishwa kwa maisha ya ndani ya wahusika ndilo jambo muhimu zaidi katika utanzu wa tamthilia. Kwa kutumia mifano kutoka kwa angalau kazi mbili ulizosoma, jadili na ulinganishe njia mbalimbali zilizotumika kuwasilisha maisha haya ya ndani.
2. Misukumo inayopingana, kama vile ubinafsi dhidi ya ukarimu, mara nyingi hutumiwa na waandishi wa tamthilia. Katika angalau tamthilia mbili ulizosoma, jadili ni kwa njia zipi waandishi wametumia misukumo kama hii ili kuimarisha kazi zao.
3. Ni nini umuhimu wa vipengele kama vile vifaa vya jukwaa na maleba (mavazi ya wasanii wakiwa kwenye onyesho) katika mchezo wa kuigiza? Linganisha jinsi vipengele hivi vilivyotumika katika angalau kazi mbili ulizosoma.

### Riwaya

4. Waandishi mara nyingi hujumuisha mbinu kama vile kisengerenyuma na/au kisengerembele. Katika kazi za angalau waandishi wawili ulizosoma, onyesha jinsi walivyotumia moja au mbinu hizi mbili kwa ufanisi.
5. Katika fasihi, safari zina malengo mengi. Linganisha jinsi safari zinavyotumika katika angalau kazi mbili ulizosoma.
6. Kazi za kifasihi mara nyingi huonyesha wahusika wakiwa katika mgogoro unaosababisha wao kuwa katika njia panda ya kutenda wema au la. Linganisha jinsi migogoro kama hii ilivyowasilishwa katika kazi za angalau waandishi wawili ulizosoma.

### Ushairi

7. “Mishororo ya mwisho wa shairi inafaa kudumu akilini mwako milele.” Jadili jinsi angalau washairi wawili wa kazi ulizosoma walivyobuni miisho yenye maana.
8. Sitiari ina jukumu gani katika kuwasilisha maisha ya mtu binafsi? Thibitisha jibu lako katika swali hili kwa kujadili kazi za angalau waandishi wawili.
9. Ni kwa njia gani mada ya kazi ya kishairi inafanikiwa kuakisi maana ya shairi? Jibu swali hili kwa kulinganisha kazi za angalau waandishi wawili ulizosoma.

### **Riwaya ya mapenzi**

- 10.** Katika uhusiano wa kimapenzi, tabia za wahusika wakati mwingine huenda kinyume na matamshi yao. Jadili utata wa sifa hizi kwa kulinganisha kazi za angalau waandishi wawili wa riwaya za mapenzi ulizosoma.
  
  - 11.** “Mateso ni mji ambao huhitaji watu wenye ujasiri.” Linganisha mbinu zilizotumiwa na angalau waandishi wawili wa kazi ulizosoma kudhihirisha ujasiri huo katika mahusiano.
  
  - 12.** Linganisha jinsi matumizi ya lugha ya kitamathali katika angalau kazi mbili ulizosoma yalivyotumiwa kwa ufanisi kudokeza hatima ya wapenzi.
-